



**TANGAZO LA NAFASI ZA KUWA MJUMBE WA KAMATI YA MKOA  
YA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA USAFIRI ARDHINI KATIKA MKOA  
RUVUMA**

**TAREHE YA KUENZA TANGAZO: 1<sup>st</sup> SEPTEMBER, 2021**

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA Consumer Consultative Council), lipo kwa mujibu wa kifungu namba 29 cha Sheria namba 3 ya LATRA ya Mwaka 2019 (CAP.413, 2019).

Kwa mujibu wa Kif. 31(1)(c), Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC) limepewa jukumu la kuunda kamati ya Mkoa itakayosimamia utekelezaji wa Majukumu ya Baraza ndani ya Mkoa kwa kujitolea.

Baraza linatangaza nafasi tano (05) za Wajumbe wa kamati ya Mkoa huu.

**MAJUKUMU YA WAJUMBE WA KAMATI ZA WATUMIAJI.**

- i. Kuelimisha watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini juu ya Haki na Wajibu wao.
- ii. Kuratibu kazi na maendeleo ya Vilabu vya wanafunzi wa Shule za msingi na sekondari.
- iii. Kufuatilia hali halisi ya usafiri ndani ya mkoa husika na kutoa taarifa kwa Katibu Mtendaji wa Baraza.
- iv. Kushirikiana na Mamlaka ya LATRA katika Mkoa husika, serikali ya Mkoa na halmashauri zake juu ya namna bora ya kuboresha huduma za usafiri kwa kuzingatia Haki na Maslahi ya mtumiaji wa Usafiri wa Ardhini.
- v. Kuwa kiungo baina ya watumiaji serikali katika mkoa husika na Baraza.
- vi. Kusambaza taarifa na maoni ya watumiaji kwa Mamlaka ya LATRA mkoani na wadau wengine.
- vii. Kufanya majukumu mengine atakayo elekezwa na Katibu Mtendaji au watakayo kubaliana kwenye kamati ya mkoa ya watumiaji kulingana na uhitaji wa mazingira na wakati husika.

## **MASLAHI YA WAJUMBE.**

Hakuna ujira. Kazi za kamati za Mkoa za watumiaji zitafanywa kwa kujitolea.

### **SIFA ZA MWOMBAJI.**

- i. Awe Mtanzania, mwenye akili timamu, mchapa kazi na mwenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea
- ii. Asiwe mmiliki wa chombo chochote cha kutoa huduma ya usafiri wa Ardhini.
- iii. Awe anaishi au ni mwajiriwa ndani ya mkoa husika
- iv. Awe mwenye nguvu, moyo na nafasi ya kujitolea kufanya kazi na kujituma kwa ajili ya kuisaidia jamii juu ya masuala yanayohusu usafiri.
- v. Awe anajua kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili na uwezo wa kuwasiliana na watu
- vi. Awe mzalendo na mwaminifu kwa mali na rasilimali za umma.
- vii. Wanawake wanahimizwa kuomba.

Mtu yeyote mwenye sifa hizo hapo juu atume maombi kwa anuani au barua pepe ya Baraza ukiambatanisha: wasifu wako (CV), Vivuli vya vyeti vya Elimu, Picha yako ya hivi karibuni (passport zize) ndani ya siku 21 tangu tarehe ya Tangazo hili.

NB: Andika namba yako ya mawasiliano. Siku ya Mahojiano na Interview utajulishwa ndani ya siku 14 baada ya kutuma maombi yako.

**Tuma kwa anuani hii**

**Katibu Mtendaji,  
Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini,  
Jengo la NSSF Waterfront ghorofa ya 7,  
S.L.P 14154  
Dar es Salaam,  
au**

**Barua pepe:** [barua@latracc.go.tz](mailto:barua@latracc.go.tz)

**Pia tembelea Tovuti:** [www.latracc.go.tz](http://www.latracc.go.tz), instergram, na tweeter:  
[latracc.go.tz](http://latracc.go.tz)

LATRA CCC NSSF Waterfront 7<sup>th</sup> Floor, Sokoine Drive, S.L.P 14154, Dar es Salaam.  
Tel: +255 22 2127410, Fax: +255 22 2127411, website: [www.latracc.go.tz](http://www.latracc.go.tz) email: [barua@latracc.go.tz](mailto:barua@latracc.go.tz)